JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

## HAIBA NA MICHEZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU

# DARAJA LA A (GATCE) 2023

# 650 HAIBA NA MICHEZO

*Kimechapishwa na;*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI.......................................................................................................... iv

1.0 UTANGULIZI ......................................................................................... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI .. 2

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI .............................. 2

2.1.1 Swali la 1: Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo ........................................................................................... 2

2.1.2 Swali la 2: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo....... 5

2.1.3 Swali la 3: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........................................................................................... 8

2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo............................................................................................ 11

2.1.5 Swali la 5: Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo ........................................................................................... 14

2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo..... 17

2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia ......................................................................................... 20

2.1.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia.................................. 23

2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo26

2.1.10 Swali la 10: Zana za Kufundishia na Kujifunzia................................ 29

2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA ............................................. 32

2.2.1 Swali la 11: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo ........................................................................................................ 32

2.2.2 Swali la 12: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo ........................................................................................................ 37

2.2.3 Swali la 13: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo ........................................................................................................ 40

2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia ......................................................................................... 46

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KATIKA KILA MADA 50

4.0 HITIMISHO ......................................................................................... 51

5.0 MAPENDEKEZO ................................................................................. 51

KIAMBATISHO CHA PEKEE ................................................................ 53

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Astashahada ya Ualimu wa Msingi katika somo la Haiba na Michezo mwaka 2023. Taarifa hii inakusudia kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza Mitaala na wadau mbalimbali wa elimu. Mtihani ni zana mojawapo inayotumika kutathmini na kutoa hitimisho katika mchakato wote wa ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo, majibu ya watahiniwa katika mtihani huonesha viwango vya uwezo wa kufikiri, ubora wa mielekeo, stadi na maarifa ambayo watahiniwa waliyapata katika miaka miwili ya mafunzo ya Ualimu.

Katika kufanya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, sababu zilizofanya watahiniwa kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu vizuri zimeainishwa. Aidha, uchambuzi wa kila mada na kiwango cha ufaulu umeambatanishwa katika kiambatisho cha pekee.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa somo hili unaonesha kuwa watahiniwa wote (asilimia 100) walikuwa na ufaulu mzuri. Sababu zilizochangia ufaulu huo ni watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizotahiniwa, umahiri wa kutosha katika kuandika hoja zenye mtiririko mzuri kimantiki na umakini katika kusoma na kuelewa matakwa ya maswali. Hata hivyo, sababu za kushindwa kujibu vizuri katika baadhi ya maswali zimeainishwa ikiwemo kutoelewa matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha katika baadhi ya mada, kutoa ufafanuzi usiotosheleza na kutokuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwenye maswali.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, mrejesho uliotolewa katika taarifa hii utasaidia kuinua kiwango cha ufaulu na kuboresha mafunzo ya Ualimu kwa ujumla hasa katika somo la Haiba na Michezo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani na wote walioshiriki katika maandalizi ya taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Astashahada ya Ualimu Daraja A mwaka 2023 kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani wa somo la Haiba na Michezo.

Maswali ya mtihani wa somo la Haiba na Michezo yaliandaliwa kutoka kwenye muhtasari wa somo la Haiba na Michezo wa mwaka 2009 na muundo wa fomati wa mwaka 2022. Maswali hayo yalihusisha mada tano zinazofundishwa katika ngazi ya cheti. Mtihani wa somo la Haiba na Michezo ulikuwa na jumla ya maswali 14 yaliyogawanywa katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 yaliyohitaji majibu mafupi na watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) ya insha na watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote.

Jumla ya watahiniwa 4,353 walifanya mtihani wa somo la Haiba na Michezo. Kiwango cha ufaulu katika mtihani huu kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walifaulu. Takwimu zinaonesha kuwa ufaulu umeendelea kuwa mzuri sawa na mwaka 2022 kama inavyoonekana katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na.1**: **Ulinganifu wa Ufaulu wa Watahiniwa kwa mwaka 2022 na 2023**

| Mwaka | Watahiniwa Waliofanya | Asilimia ya Watahiniwa Waliofaulu | Madaraja (Asilimia) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | A | B | C | D |
| 2022 | 3,273 | 100.00 | 106 (3.2%) | 2,090 (64.3%) | 1,048 (32.3%) | 6 (0.2%) |
| 2023 | 4,353 | 100.00 | 65 (1.5%) | 2,523 (58.6%) | 1,710 (39.7%) | 7 (0.2%) |

Jedwali Na.1 linaonesha kuwa, 1.5% ya watahiniwa walipata daraja A, 58.6% daraja B, 39.7% daraja C na 0.2% daraja D kwa mwaka 2023. Aidha, ufaulu wa watahiniwa kwa daraja A na B umeshuka ukilinganishwa na mwaka 2022. Ufaulu wa daraja C umeongezeka kwa asilimia 7.4 kutoka 32.3 hadi asilimia 39.7 mwaka 2023.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni ufaulu mzuri, wastani na hafifu. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69 na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, kiwango cha

ufaulu kwa kila swali katika sehemu A ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata alama 3 hadi 4, kiwango cha *wastani* alama 2 hadi 2.5 na kiwango *hafifu* alama 0 hadi 1.5. Kwa maswali ya sehemu B, kiwango cha ufaulu katika kila swali ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata alama 10.5 hadi 15, kiwango cha *wastani* alama 6 hadi 10 na kiwango *hafifu* alama 0 hadi 5.5.

Katika kufanya uchambuzi na kutafsiri ufaulu wa watahiniwa, chati na rangi zimetumika ili kufafanua ufaulu husika. Rangi ya kijani, njano na nyekundu zimetumika kwenye chati na kwenye kiambatanisho cha pekee kuonesha ufaulu mzuri, wastani na hafifu mtawalia. Taarifa hii imeeleza pia sababu za watahiniwa kujibu vizuri au kushindwa kujibu vizuri. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa zimetumika kama vielelezo katika kuonesha mifano halisi ya hoja zilizoainishwa.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Maswali katika sehemu A yalitoka katika mada tano (5) ambazo ni *Zana za Kufundishia na Kujifunzia; Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia; Maandalizi ya Ufundishaji; Misingi ya Kufundishia Somo la Haiba na Michezo* na *Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo*. Kila swali lilikuwa na jumla ya alama nne (4) hivyo kufanya jumla ya alama arobaini (40) katika sehemu hii.

#### 2.1.1 Swali la 1: Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi tofauti mbili zilizopo kati ya upimaji na tathmini. Lengo la swali hili lilikuwa ni kupima uwezo wa watahiniwa katika kukumbuka dhana hizo na kuweza kuzitofautisha. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 1,677 (38.5%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 2,555 (58.7%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 121 (2.8%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu 97.2% ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu ni kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.




**Chati Na.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kati ya watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4, asilimia 4.9 walipata alama zote nne. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika kutofautisha upimaji na tathmini. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitofautisha dhana hizo kwa usahihi kama ifuatavyo: *upimaji ni kitendo cha kutaka kujua ni kwa kiasi gani mwanafunzi ameweza kupata maarifa katika ufundishaji na ujifunzaji* wakati *tathmini ni utaratibu wa kuchunguza hali halisi kwa lengo la kupata data zitakazowezesha kufanya uboreshaji na urekebishaji wa mambo mbalimbali ya kielimu*. Kielelezo Na.1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



| 1 | |
|---|---|
| Upimaji | Tathmini |
| - Ni kitendo cha mwalimu kutaka kujua ni kwa kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa, stadi na ujuzi kulingana na nyanja za upimaji | - Ni mchakato wa kutaka kujua ni kwa kiasi ~~malo~~ malengo yamefanikiwa au hayajafanikiwa na mara nyingi huambatana na maamzi. |
| - Hutumia nyanya za upimaji kuchunguza tatizo mfano mazoezi, majaribio na mitihani | - Hutumia data zilizo-patikana kutokana na nyanja za upimaji zilizo tumika kutatua tatizo |

**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi tofauti ya upimaji na tathmini katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walitoa hoja pungufu na kuandika baadhi ya hoja zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *Upimaji ni kutafuta ni kwa kiasi gani ameweza kupata maarifa na stadi zilizokusudiwa katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji lakini Tathmini ni utaratibu wa kufanya uchunguzi na udadisi na kutoa matokeo katika kutafuta ufikiwaji wa ufundishaji na ujifunzaji.* Mtahiniwa huyo alitoa hoja pungufu hivyo hazikukidhi matakwa ya swali. Mtahiniwa mwingine aliandika majibu kama: *Upimaji unasaidia kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi* wakati *tathmini inasaidia kuweka wanafunzi madarasa tofauti tofauti*, vile vile *upimaji husaidia kujua wanafunzi wenye mahitaji maalum* wakati *tathmini inasaidia uthibiti viwango vya elimu na mtaala wake.* Mtahiniwa alitoa maelezo sahihi upande wa upimaji lakini upande wa tathmini maelezo hayakuwa sahihi. Majibu hayo yanaonesha kuwa, watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tofauti zilizopo kati ya dhana ya Upimaji na Tathmini.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 walikuwa na uelewa mdogo kuhusu dhana ya Upimaji na Tathmini. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitofautisha dhana hizo kwa kuandika: *tathmini husaidia kutathmini kiwango cha ubora elimu inayotolewa, upimaji huonesha nafasi ya mwanafunzi wakati tathmini huonesha nafasi ya mwanafunzi, upimaji hupimwa kwa kutumia zana za upimaji, katika tathmini taarifa hukusanywa kwa kutumia matokeo ya upimaji, upimaji husaidia kujua maendeleo ya wanafunzi kitaaluma.* Mtahiniwa huyo alieleza utofauti wa dhana kiujumla katika muktadha wa elimu badala ya tofauti ya dhana hizo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



1.

Haiba Ni ile namna ya Mwalimu kumwangalia Mwanafunzi juu ya Uwezo, Nidhamu Katika Ufundishaji na Ujifunzaji.

Michezo Ni ile namna ya Mwalimu kukuza kipaji au stadi mbalimba za maisha katika Ufundishaji na Ujifunzaji.

**Kielelezo Na. 1.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.2, mtahiniwa alieleza maana ya haiba na maana ya michezo badala ya kueleza tofauti iliyopo kati ya Upimaji na Tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.1.2 Swali la 2: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutaja sifa nne zinazobainisha ubora wa sauti ya mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Lengo la swali hili lilikuwa ni kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu ubora wa sauti ya mwalimu katika ufundishaji. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 2,528 (58.1%) walipata alama 3 hadi 4,

watahiniwa 1,053 (24.2%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 772 (17.7%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 82.3 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na.2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, kati ya watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4, asilimia 27 walipata alama zote katika swali hili. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha na walielewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kama ifuatavyo: *sauti isikike vizuri, iwe ya kirafiki na inayohamasisha, iwe inayoeleweka vizuri, iwe inayofuata taratibu za uzungumzaji mfano kufuata alama za uandishi, iwe ya kutoa hamasa kwa wanafunzi kuzungumza, kutamka maneno kwa usahihi na kwa ufasaha*. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



2 i) Sauti iwe inasikika vizuri ili kuvuta usikivu wa Mwanafunzi.
ii) Sauti iwe na Mpangilio Mzuri wa Maneno ili kuwafanya wanafunzi kusikiliza vizuri.
iii) Sauti iwe na Matamshi sahihi wa Maneno ili kuweza kueleweka kwa wanafunzi.
iv) Sauti iwe inavutia ili kuamsha ari ya kujifunza kwa Mwanafunzi.

**Kielelezo Na. 2.1**: Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi sifa nne zinazobainisha ubora wa sauti ya mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walitoa baadhi ya hoja zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *utamkaji wa maneno kwa usahihi, uwe ya kuzingatia lafudhi sahihi ya lugha, iwe inasikika vizuri kwa wanafunzi wote* na *mwalimu azungumze kwa kujiamini.* Katika majibu hayo, hoja ya kwanza na ya tatu ni sahihi, lakini hoja ya pili na ya nne sio sahihi. Mtahiniwa mwingine, aliandika majibu kama: *utamkaji sahihi wa maneno, isiwe lugha ya matusi, isikike vizuri kwa wanafunzi na isiwe kubwa sana.* Hoja ya kwanza na ya tatu ni sahihi wakati hoja ya pili na ya nne hazikuwa sahihi. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa za sauti ya mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuwa na maarifa kuhusu ubora wa sauti ya mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Pia, hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kuandika majibu yanayolenga ujuzi wa mwalimu katika kuandaa somo badala ya ubora wa sauti ya mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Mfano wa majibu hayo ni: *kujiamini, umahiri wake katika kufundisha somo, matumizi ya zana, uwezo wa kuandaa azimio la kazi na andalio la somo*. Mtahiniwa mwingine aliandika majibu kama: *isiwe ya upole, sauti isiwe na mikwaruzo, sauti inapaswa isiwe ya kuumiza masikio, sauti yenye hoja inayoeleweka kwa wanafunzi.* Majibu hayo yanaonesha watahiniwa

hawakuwa na maarifa kuhusu ubora wa sauti ya mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


2

i) uwezo wa kujiamini · mwalimu anaejiamini hu
wa na sauti bora

ii) umahili wake katika kufundisha somo

iii) Matumizi ya zana

iv) uwezo wa kuandaa azimio la kazi na and-
alio la somo.

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa alieleza ujuzi wa mwalimu katika kufanya maandalizi ya ufundishaji badala ya sifa za ubora wa sauti ya mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.1.3 Swali la 3: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi matumizi manne ya kitabu cha Kiongozi cha Mwalimu. Lengo la swali hili lilikuwa ni kupima uwezo wa watahiniwa katika kukitumia Kiongozi cha Mwalimu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 4,338 (99.7%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 10 (0.2%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 5 (0.1%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 99.9 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na.2.

**Jedwali Na.2: Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3**

| Alama | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| 0.0 - 1.5 | 5 | 0.1 |
| 2.0 - 2.5 | 10 | 0.2 |
| 3.0 - 4.0 | 4338 | 99.7 |

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kati ya watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4, asilimia 96.4 walipata alama zote nne katika swali hili. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya matumizi ya Kiongozi cha Mwalimu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kama ifuatavyo: *humuongoza mwalimu katika kubaini zana za kufundishia na kujifunzia, humuongoza mwalimu katika kubaini maswali na mazoezi mbalimbali, huonesha majibu ya maswali ya mazoezi, huonesha mbinu na njia za kufundishia mada husika.* Kielelezo Na. 3 1 ni sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3.


3

(i) Kwa sababu huonyesha njia/mbinu ambazo mwalimu atatumia wakati wa ufundishaji mfano majadiliano katika vikundi.

(ii) Huonyesha mada kwa mtiririko ambazo zipo katika muhtasari na kitabu cha kiada

(iii) Huonyesha zana za kufundishia kulingana na malengo mahususi yanayopimwa au yanayofundishwa.

(iv) Huonyesha majibu ya maswali yaliyo katika kitabu cha kiada ambapo huwa rahisi kwa mwalimu katika kusahihisha kazi za wanafunzi mfano mazoezi.

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3

Katika Kielelezo Na. 3.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi matumizi ya Kiongozi cha Mwalimu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walitoa baadhi ya hoja zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *humsaidia mwalimu kujua mada atakazofundisha, humsaidia mwalimu kupata maelekezo zaidi kwa kila mada, humsaidia mwalimu kujua zana za kufundishia na kujifunzia na humsaidia mwalimu kujua mada zilivyopangwa vizuri.* Katika majibu ya mtahiniwa huyo, hoja ya pili na ya tatu ni sahihi, wakati hoja ya kwanza na ya nne sio sahihi. Majibu hayo ya mtahiniwa yanaonesha kuwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu matumizi ya Kiongozi cha Mwalimu.

Pamoja na ufaulu kuwa mzuri, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 walitoa baadhi ya hoja zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kama ifuatavyo: *kiendane na umri wa walengwa, kiendane na mada ya somo husika, kiwe au kioneshe mbinu za kufundishia na kujifunzia.* Katika majibu ya mtahiniwa, hoja ya tatu ilikuwa sahihi wakati hoja ya kwanza na ya pili hazikuwa sahihi kwa kuwa alieleza sifa za maandiko rejea badala ya matumizi ya Kiongozi cha Mwalimu. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.


3
i) kiongozi cha mwalimu humpatia farahasa ya maneno mpya. mwalimu kwa ajili ya kufundishia.
ii) kiongozi cha mwalimu humsaidia mwalimu kujua mada zinazotakiwa kufundishwa kwa somo husika.
iii) kiongozi cha mwalimu husaidia kuonyesha mtiririko wa mada
iv) kiongozi cha mwalimu husaidia kuonyesha lugha fasaha ya maneno

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3

Katika Kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alieleza kuhusu muhtasari wa somo katika baadhi ya hoja na kitabu cha kiada katika hoja nyingine badala ya matumizi ya Kiongozi cha Mwalimu.

### 2.1.4 Swali la 4: Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi tofauti nne zilizopo kati ya mpira wa kikapu na mpira wa pete. Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika kukumbuka dhana hizo na kuweza kuzitofautisha. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 629 (14.3%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 1,304 (30%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2,420 (55.6%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwa sababu asilimia 44.4 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na.3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuwa na maarifa kuhusu mpira wa kikapu na mpira wa pete hivyo walishindwa kutofautisha dhana hizo. Aidha, watahiniwa wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali hilo hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja zisizo

sahihi kama ifuatavyo: *mpira wa kikapu wachezaji huvaa nguo kubwa wakati wa kucheza wakati mpira wa pete wachezaji huvaa nguo za kubana, mpira wa kikapu una jumla ya wachezaji kumi na nane wakati mpira wa pete una jumla ya wachezaji kumi na mbili*. Mtahiniwa mwingine alitoa maelezo yasiyo sahihi kama vile: *mpira wa kikapu huwa na wachezaji kumi na nne kila timu wachezaji saba, mpira kwa pete huchezwa na watu kumi na mbili kila timu wachezaji sita, mpira wa kikapu kuna watu maalumu wa kufunga lakini mpira wa pete hakuna watu maalumu wa kufunga*. Mtahiniwa huyo alichanganya majibu sahihi ya mpira wa pete kwa kuyaandika kwenye mpira wa kikapu mfano, *mpira wa kikapu huwa na wachezaji kumi na nne kila timu wachezaji saba* na *mpira wa kikapu kuna watu maalumu wa kufunga lakini mpira wa pete hakuna watu maalumu wa kufunga* hayo ni majibu sahihi upande wa mpira wa pete. Halikadhalika jibu moja sahihi upande wa mpira wa kikapu liliandikwa kwenye mpira wa pete mfano, *mpira wa pete hakuna watu maalumu wa kufunga*. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya jibu lisilo sahihi.


4
i) Mchezo wa kikapu huchezwa na wachezaji kumi na nane Lakini mchezo wa pete huchezwa na wachezaji ishirini

ii) Mchezo wa kikapu unatundu kubwa la kufungia gori lakini Mchezo wa pete unatundu dogo la kufungia gori

iii) Mchezo wa kikapu hutumia muda mwi-ngi kuchezwa lakini mchezo wa pete hutumia muda mchache kuchezwa

iv) Mchezo wa kikapu magori yake ni mara-fu sana lakini mpira wa pete magori yake ni ya wastani

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4

Katika Kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa alitoa tofauti zisizo sahihi kati ya mpira wa kikapu na mpira wa pete. Mtahiniwa alielewa matakwa ya swali lakini hakuwa na maarifa kuhusu dhana hizo.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walitoa hoja pungufu na kuandika baadhi ya hoja zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitofautisha dhana hizo kama vile: *mpira wa kikapu huwa na wachezaji watano kila upande* lakini *mpira wa pete huwa na wachezaji saba kila upande*. *Mpira wa kikapu huwa na sheria zake* lakini *mpira wa pete huwa na sheria zake*. Mtahiniwa huyo alitoa tofauti ya kwanza ambayo ni sahihi lakini tofauti ya pili haikuwa sahihi. Mtahiniwa mwingine aliandika majibu kama: *mpira wa kikapu huchezwa kwa kota tatu tofauti* lakini *pira wa pete huchezwa kwa nusu mbili. Mpira wa kikapu huchezwa na wachezaji wa jinsi zote* lakini *mpira wa pete huchezwa na wanawake tu.* Mtahiniwa huyo pia alitoa tofauti ya kwanza isiyo sahihi lakini tofauti ya pili ilikuwa sahihi. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa, watahiniwa wengi katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tofauti zilizopo kati ya mpira wa pete na mpira wa kikapu.

Pamoja na ufaulu kuwa hafifu katika swali hili, wapo watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4. Kati yao, asilimia 2.1 walipata alama zote nne katika swali hili. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali na walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tofauti za michezo hiyo. Baadhi ya majibu waliyotoa ni kama ifuatavyo: *mpira wa kikapu una wachezaji watano kwa kila timu* wakati *mpira wa pete una wachezaji saba kwa kila timu, mpira wa kikapu mchezaji yeyote anaweza kufunga lakini mpira wa pete una wafungaji maalum, mpira wa pete mfungaji akifunga linahesabika goli moja wakati mpira wa kikapu inategemea eneo alilofungia mchezaji, mpira wa pete wachezaji wana mipaka maalum ya kucheza wakati mpira wa kikapu mchezaji anaweza kucheza eneo lolote la uwanja, mpira wa kikapu huchezwa kwa kudundisha mpira chini* wakati *mpira wa pete huchezwa kwa kurusha mpira*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya jibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


4 i) Mchezo wa mpira wa kikapu unachezwa kwa kudunda na kutoa pasi lakini mchezo wa mpira wa pete unachezwa kwa kupeana pasi
ii) Mchezo wa mpira wa kikapu una wachezaji watano kwa kila timu lakini Mchezo wa pete Una wachezaji saba kwa kila timu
iii) Mchezo wa mpira wa kikapu hauna majina ya wachezaji lakini mchezo wa mpira wa pete Una majina ya wachezaji mfano C – center
iv) Mchezo wa mpira wa kikapu ~~hauna shoti~~ Una shoti ya kupiga hatua tatu ukiwa na mpira lakini pete hauruhusiwi kutembea wala kupiga hatua ata moja

**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 4

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa alitofautisha kwa usahihi mpira wa kikapu na mpira wa pete.

### 2.1.5 Swali la 5: Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutaja sifa nne za mrejesho wenye ubora kwa wanafunzi wa somo la Haiba na Michezo. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 59 (1.3%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 586 (13.5%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 3,708 (85.2%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwa sababu asilimia 14.8 ya watahiniwa ndio waliofaulu kwa kupata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu katika swali hili ni kama inavyoonekana katika Chati Na.4.




**Chati Na. 4***: Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa juu ya sifa za mrejesho wenye ubora kwa wanafunzi wa somo la Haiba na Michezo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama ifuatavyo: *uwe unaendana na umri na uwezo wa wahusika, uwe unazingatia mazingira ya kufanyia tathmini, usiwe na upendeleo ndani yake* na *upime Nyanja zote za utambuzi.* Mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi kama: *uwepo wa alama za kila swali, uwepo wa alama za jumla za upimaji, uwepo wa matokeo ya upimaji, kuwepo kwa mwongozo wa usahihishaji na kuonyesha alama za kila mwanafunzi*. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.

**5**

i) Ni lazima mwanafunzi atunukiwe cheti; amba po mwanafunzi anapopimwa huambatanishwa na cheti chake.

ii) Ni lazima utoe ripoti ya maendeleo ya mwanafunzi; ambapo mwanafunzi anapopimwa huweza kuwapatia wazazi ripoti ya maende leo ya mwanafunzi.

iii) Humpa mwanafunzi nafasi ya kuendelea na ngazi nyingine ya elimu; mfano kutoka kidato cha nne kwenda kidato cha sita.

iv) Huwasaidia walimu kuwapanga wanafunzi katika mikondo; ambapo upimaji unapofanyika huweza kuwapanga wanafunzi katika mikondo mbalimbali.

Kielelezo **Na. 5.1:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa alieleza faida za Upimaji na Tathmini kwa ujumla badala ya sifa za mrejesho wenye ubora toka kwa mwalimu kwenda kwa mwanafunzi.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 umeonesha kuwa, walichanganya dhana ya upimaji na tathmini na mrejesho wenye ubora kutoka kwa mwalimu baada ya upimaji. Kwa mfano, mtahiniwa aliandika; *uoneshe kufikika kwa malengo ya somo, usiwe na changamoto kwa walengwa/wanafunzi, uwe na matokeo au alama nzuri mfano A na B, uoneshe ubora wa mbinu za zana zilizotumiwa* na *mwalimu katika kufundishia na kujifunzia.* Katika majibu ya mtahiniwa, hoja ya pili na ya tatu zinaongelea upimaji na tathmini badala ya mrejesho wenye ubora kwa wanafunzi wa somo la Haiba na Michezo ili kuboresha ujifunzaji wao. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa, hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Upimaji na Tathmini.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 walieleza kwa ufasaha sifa za mrejesho wenye ubora kwa wanafunzi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wao. Kati yao, asilimia 0.2 walielewa matakwa ya

swali, hivyo kufafanua kwa usahihi hoja zote nne. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa za mrejesho wenye ubora kwa wanafunzi ili kuboresha ujifunzaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *mrejesho wenye ubora lazima uwe na muda maalum, mrejesho wenye ubora lazima uoneshe walengwa, mrejesho wenye ubora lazima upimike, mrejesho wenye ubora lazima uwe na uhalisia, uhusiane na lengo mahsusi, ulenge somo na sio haiba au mambo ya familia, utolewe kwa uharaka na uhamasishe walengwa katika kujifunza*. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


5 Mrejeho katika upimaji wa somo Katika Ufundishaji na ujifunzaji:
(a) kufikiwa kwa malengo mahususi aliyotarajiwa kupimwa.
(b) Kuboresha kwa Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji mara baada ya upimaji.
(c) Ushiriki wa Wanafunzi katika kutoa /kujibu maswali mbalimbali.
(d) Mrejesho wa kubaini changamoto zinazowakabili wanafunzi katika kujifunza na Namna ya kutatua changamoto hizo.

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alieleza kwa ufasaha sifa zote za mrejesho wenye ubora kwa wanafunzi wa somo la Haiba na Michezo ili kuboresha ujifunzaji.

### 2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi mada nne ambazo mwanafunzi anaweza kujifunza kwa kutumia msingi wa ujifunzaji kwa vitendo. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walijibu swali hili ambapo watahiniwa 1,687 (38.8%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 1,317 (31.3%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1,302 (29.9%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla ufaulu wa swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa

asilimia 70.1 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na.5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 walibainisha kwa ufasaha mada ambazo wanafunzi wanaweza kujifunza kwa kutumia msingi wa vitendo. Kati yao, asilimia 11.2 walielewa matakwa ya swali, hivyo kubainisha kwa usahihi mada zote nne ambazo mwalimu anaweza kuwafundisha wanafunzi kwa kutumia msingi wa vitendo. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa ni kama: *michezo sahili, mada ya mchezo wa soka, michezo ya jadi, mada ya kucheza michezo ya kuvuta kamba, mada inayohusu maswala ya riadha.* Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


6

i) Mada ya Michezo sahili mfano Rede, nasaka Mke wangu

ii) Mada ya Michezo ya Mipira Mfano Mpira wa Miguu, pete, Mpira wa ~~Mel~~ Kikapu na Mpira wa Volebo.

iii) Mada ya Michezo ya Riadha mfano Miruko, Mitupo na kukimbia.

iv) Mada ya Michezo ya asili Mfano bao, Drafiti.

v) Mada ya michezo ya jadi mfano Mchezo wa ~~Ngoma~~ ngoma, Sindimba

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6

Katika kielelezo Na. 6.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi mada zote nne ambazo mwanafunzi anaweza kujifunza kwa kutumia msingi wa vitendo.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walibainisha mada mbili badala ya nne zilizotakiwa katika swali na wengine walishindwa kueleza kwa usahihi mada walizoziorodhesha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *Michezo mbalimbali kama riadha, michezo ya mpira, utumiaji wa vifaa vya michezo, maandalizi ya ufundishaji* na *michezo sahili.* Katika majibu ya mtahiniwa huyo hoja ya kwanza, ya pili na ya nne hakuzitolea maelezo wakati hoja ya tatu haikuwa sahihi. Mtahiniwa mwingine aliandika: *mchezo wa mpira, mchezo wa kuvuta Kamba, mchezo wa mbio* na *mchezo wa rede.* Mtahiniwa huyo aliorodhesha mada sahihi lakini hakutoa maelezo kuhusu mada hizo, hivyo alipata alama mbili badala ya alama zote nne katika swali hilo. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa, watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada zote ambazo mwanafunzi anaweza kujifunza kwa kutumia msingi wa vitendo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Asilimia 4 ya watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali na miongoni mwao hawakuwa na maarifa kabisa kuhusu dhana zilizoulizwa, hivyo walipata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu

kama: *maadili na utu, utamaduni, fikra yakinifu* na *mahusiano mema, uwajibikaji, kujithamini na kuwathamini wengine, afya na michezo, mada ya ubunifu, usafi wa mwili, mada ya usafi wa mazingira, mada ya upishi, mada ya ushonaji, ushiriki wa wanafunzi na tabia zao, mada ya haiba.* Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.


6
i) Mada ya Stadi ya Maisha ambayo imegawanyika - Katika Sehemu Kuu mbili Stadi za Maisha za Kufikiri Kujitambua na Kujenga Uthubutu.
ii) Mada ya Ufundishaji na Ujifunzaji, Mwanafunzi atajifunza kwa vitendo namna ya Kuandaa Maandalio ya somo na Maazimio la Kazi.
iii) Mada ya tathmini ambapo atapata, kufanya data katika mdakato wa Kufanya tathmini
iv) Katika Mitaala wa Ufundishaji Unaozingatia Kufanya vipi vya Mtu mmoja mmoja na timu Kwa Ujumla.

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alitaja mada ambazo hazipo kwenye somo la Haiba na Michezo badala ya kueleza mada zilizopo kwenye somo hilo ambazo mwanafunzi anaweza kujifunza kwa kutumia msingi wa vitendo.

### 2.1.7 Swali la 7: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha vifaa vinne vinavyohitajika katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo. Lengo la swali hili lilikuwa ni kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutumia vifaa mbalimbali vya mtaala katika ufundishaji. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote 4,353 (100%) ambapo watahiniwa 1,192 (27.4%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 1,835 (42.1%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1,326 (30.5%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa, asilimia 69.5 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata alama

2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na.6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuwa na maarifa kuhusu mada ya maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kushindwa kutoa majibu sahihi. Kwa mfano, mtaniniwa mmoja aliandika vitu vinavyomwezesha kuandaa somo badala ya vifaa vya mtaala kama vile: *tini za masomo*, *zana za kufundishia na kujifunzia*, *kalenda ya shule, rejea, machapisho mbalimbali*. Aidha, mtahiniwa mwingine alibainisha vifaa visivyo sahihi kama: *filimbi, jezi, kadi mbalimbali, nguo za michezo, viwanja vya kila michezo.* Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


7
(i) Andalio la somo
(ii) Azimio la kazi
(iii) Shajara
(iv) Nukuu za somo

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7

Katika Kielelezo Na. 7.1, mtahiniwa alitaja vifaa ambavyo mwalimu anapaswa kuviandaa kabla ya kufundisha badala ya kutaja vifaa vya mtaala vinavyoweza kutumika kufundishia somo la Haiba na Michezo.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walibainisha vifaa viwili kati ya vinne vilivyotakiwa katika swali na wengine walishindwa kueleza kwa usahihi vifaa vilivyoorodheshwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *Muhtasari, Kiongozi cha mwalimu, kitabu cha kiada* na *kitabu cha ziada.* Mtahiniwa huyo aliorodhesha vifaa sahihi lakini hakutoa maelezo kuhusu vifaa hivyo. Mtahiniwa mwingine aliandika: *muhtasari wa somo la Haiba na Michezo huwa na ufupisho juu ya mada za somo la Haiba na Michezo, kitabu cha kiada, kiongozi cha mwalimu* na *kitabu cha ziada.* Mtahiniwa alitaja hoja zilizo sahihi lakini hakuzitolea maelezo, hivyo alipata alama mbili na nusu badala ya alama zote nne. Majibu haya yanaonesha kuwa, watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia. Kati yao, asilimia 20.9 walibainisha kwa usahihi vifaa vya mtaala vinne vinavyohitajika katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo hivyo walipata alama zote 4. Majibu sahihi yaliyoandikwa ni kama: *Muhtasari wa somo ambao ni mwongozo unaochambua kwa ufupi mambo yote yanayotakiwa kufundishwa, kitabu cha kiada kinachoendana na muhtasari na kinatumiwa na mwalimu pamoja na mwanafunzi, kiongozi cha mwalimu kinachomwelekeza mwalimu mbinu anazotakiwa kutumia na hatua za ufundishaji, kitabu cha mwalimu*

*kinachotoa maelekezo ya kina kuhusu ufundishaji wa somo husika.* Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.



7

(i) Muhtasari wa somo la haiba na michezo
- Kinamwongoza mwalimu wa somo kitu cha kufundisha kwa mwezi au mwaka.
(ii) Kitabu cha kiada cha somo la haiba na Michezo
- Kitabu hiki hufafanua maudhui yote katika muhtasari wa somo la haiba na michezo.
(iii) Kiongozi cha mwalimu. cha somo la haiba na Michezo
- Humwelekeza mwalimu katika kuandaa njia na zana za kufundishia somo lake.
(iv) Kitabu cha ziada cha somo la haiba na Michezo.
- Kitabu hiki kinatoa mazoezi na maelekezo ya ziada katika somo la haiba na michezo

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya jibu lililo sahihi katika swali la 7

Katika Kielelezo Na. 7.2, mtahiniwa alieleza kwa usahihi vifaa vinne vinavyoweza kutumika katika kufundishia somo la Haiba na Michezo.

### 2.1.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi mbinu nne zinazoweza kutumika kupata zana za kufundishia na kujifunzia. Lengo la swali hili lilikuwa ni kupima uwezo wa watahiniwa kuchambua mbinu mbalimbali za kupata zana za kufundishia na kujifunzia katika mazingira yanayomzunguka mwalimu wa somo la Haiba na Michezo. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walijibu swali hili, ambapo watahiniwa 4,257 (97.8%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 752 (17.3%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 96 (2.2%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 97.8 ya watahiniwa walifaulu kwa

kupata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na.7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 walikuwa na maarifa ya kutosha hususani katika mada ndogo ya *Upatikanaji wa Zana* pamoja na kuelewa vizuri matakwa ya swali. Kati ya watahiniwa hao, asilimia 59.9 walieleza kwa usahihi mbinu nne zinazoweza kutumika kupata zana za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu sahihi kama: *mwalimu anaweza kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa kununua dukani, mwalimu anaweza kupata zana za kufundishia na kujifunzia kwa kuazima kutoka shule jirani, mwalimu anaweza kupata zana kwa kuokoteza, mwalimu anaweza kutengeneza zana kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika mazingira yetu.* Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.



8 (a) Kununua; Zana zinaweza kupatikana kwa kununua dukani mfano wa zana hizo ni Simu, Taa na vitabu.

(b) Kuokota kutoka kwenye mazingira; Mwalimu anaweza kuokota zana kama vile vijiti, mawe na maua.

(c) Kuazima; Baadhi ya zana unaweza kuazima kutoka kwa walimu wengine mfano Kompyuta.

(d) Kufaragua; Kufaragua ni kitendo cha kutumia makumi yasiyo halisi kutengeneza mfano wa kitu halisi kwa mfano kutengeneza kifani cha gari kwa kutumia maboksi.

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi mbinu nne ambazo mwalimu wa somo la Haiba na Michezo anaweza kuzitumia katika kujipatia zana za kufundishia na kujifunzia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walieleza mbinu mbili kati ya nne zilizotakiwa katika swali na wengine walishindwa kueleza kwa usahihi mbinu zilizoorodheshwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *kutengeneza, kufaragua, kununua* na *kuchora.* Mtahiniwa huyo aliorodhesha mbinu lakini hakutoa maelezo kuhusu mbinu hizo, hivyo, alipata alama mbili na nusu badala ya alama zote nne. Majibu hayo yanaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na uelewa juu ya dhana husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama:

*kuwashirikisha wazazi na wanafunzi katika kupata zana, kuomba misaada mbalimbali hata kwa shule zilizopo jirani, kuwapa mbinu ya kutumia vipaji au ubunifu ili kupata zana, kuwashirikisha wanafunzi kutafuta zana.* Mtahiniwa mwingine aliandika hoja zinazohusu vigezo vya uchaguzi wa zana badala ya mbinu za upatikanaji wa zana kama vile *kutambua malengo mahsusi, umri wa walengwa, idadi ya wanafunzi, zingatia ukubwa wa darasa je zana utakazotumia zitaonekana vizuri*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.


8

(i) Majadiliano katika vikundi:
Kuwagawa wanafunzi katika vikundi na kuwapa kazi ya kufanya kwa usimamizi.

(ii) Ziara mafunzo.
Kuwatoa wanafunzi kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine ili kujifunza.

(iii) Kazi mradi.
Ni mbinu ambayo kuanzisha jambo na baadae kuona matunda yake.

(iv) Muhadhara.
Ni mbinu ambayo mwalimu huwa mtendaji wanafunzi kusikiliza kile anachofanya mwalimu.

**Kielelezo Na. 8.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa alieleza mbinu za kufundishia na kujifunzia badala ya mbinu za kupata zana za kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo.

### 2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kufafanua kwa ufupi stadi nne za msingi ambazo mwanafunzi anatakiwa kuwa nazo ili kumwezesha kucheza mpira wa miguu kwa ufanisi. Swali hili lililenga kupima matumizi ya stadi zitakazomwezesha mchezaji kucheza mpira wa miguu kwa ufanisi. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa

1,200 (27.6%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 683 (15.7%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2,470 (56.7%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa sababu asilimia 43.3 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu ni kama inavyoonekana katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa kuhusu stadi za uchezaji wa mpira wa miguu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zinazohusu stadi za maisha badala ya stadi za mpira wa miguu kama vile: *stadi ya upendo, stadi ya kujiamini, maamuzi ya busara, ushirikiano, stadi ya kuwasiliana, stadi ya kuthubutu*. Aidha, mtahiniwa mwingine alitaja taratibu zinazotawala michezo mingi ambazo ni: *kutambua sheria na kanuni, kutambua mipaka ya uwanja, kutambua muda ambao hutumika katika mchezo, kupasha mwili joto* na *kufundisha kutofanya madhambi ya lazima.* Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



9
i) Stadi za Kujiamini; hii ni stadi ambayo inawezesha kukufanya kufanya jambo kwa ujasiti wa hali ya juu
ii) Stadi za ubunifu; Hii ni stadi ambayo huwezesha namna ya kutumia mbinu mbalimbali katika mchezo ili kuleta ushindi.
iii) Stadi za kuwasiliana; hii ni stadi muhimu ambayo huwaunganisha wachezaji ili waweze kucheza kwa ushirikiano.
iv) stadi za uthubutu; hii ni stadi ambayo wachezaji wanatakiwa kuzingatia ili kuleta mahusiano mema miongoni mwao.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9

Katika Kielelezo Na. 9.1, mtahiniwa alieleza kuhusu stadi za maisha badala ya stadi za mpira wa miguu.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 walieleza stadi mbili kati ya nne zilizotakiwa katika swali na wengine walishindwa kueleza kwa usahihi stadi zilizoorodheshwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *kufunga goli- mwanafunzi aelezwe namna ya kufunga goli, stadi ya kupiga pasi ndefu na fupi- mwanafunzi afundishwe namna ya kupiga mpira kwa usahihi, stadi ya kukabiliana na adui- mwanafunzi aelezwe namna sahihi ya kumkabili adui yake* na *stadi ya kutuliza mpira-mwanafunzi afundishwe namna ya kutuliza mpira na kumpa mchezaji mwingine.* Hoja ya kwanza na ya pili ni sahihi lakini hoja ya tatu na ya nne hazikuwa sahihi, hivyo alipata alama mbili na nusu (2.5) badala ya alama zote nne (4) katika swali hilo. Majibu hayo yanaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu stadi za mpira wa miguu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 3 hadi 4 walieleza kwa ufasaha stadi nne ambazo zitamwezesha mchezaji wa mpira wa miguu kucheza kwa ufanisi. Kati yao, asilimia 7.9 walipata alama zote nne.

Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya stadi za msingi ambazo mwanafunzi lazima awe nazo ili kumwezesha kucheza mpira wa miguu kwa ufanisi. Baadhi ya majibu sahihi yaliyoandikwa na watahiniwa ni kama: *kutoa na kupokea pasi kwa usahihi wakati wa kucheza, namna ya kumiliki mpira, kutengeneza nafasi, jinsi ya kufunga goli, jinsi ya kudaka mpira* na *jinsi ya kurusha mpira.* Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


9

i) Stadi ya kupokea na kutoa pasi: ni muhimu kufundishwa ili mwanafunzi awe na umahiri wa kupokea pasi kwa ustadi na kutoa pasi kwa ustadi.

ii) Stadi ya kumiliki mpira: Hii ni stadi ambayo ni muhimu kufundishwa ili wanafunzi wapate uwezo wa kukaa na mpira mguuni pasipo kunyang'anywa kirahisi.

iii) Stadi ya kutengeneza nafasi: Ni muhimu kufundishwa kutengeneza nafasi mbalimbali za magoli kwa wafungaji ili kuweza kufunga magoli.

iv) Stadi ya kufunga goli: Ni muhimu kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufunga goli wanapopata nafasi ya kufunga na namna ya kukaa katika nafasi ili ufunge.

**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa alifafanua kwa usahihi stadi za msingi ambazo mwanafunzi lazima awe nazo ili kumwezesha kucheza mpira wa miguu kwa ufanisi.

### 2.1.10 Swali la 10: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha faida nne anazopata mwanafunzi anapojifunza kwa kutumia zana. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 4,283 (98.3%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 68 (1.6%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2 (0.1%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani asilimia 99.9 ya watahiniwa walifaulu swali hili kwa kupata

alama 2 hadi 4. Muhtasari wa viwango vya ufaulu katika swali hili ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10**

| Alama | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| 0.0 - 1.5 | 2 | 0.1 |
| 2.0 - 2.5 | 68 | 1.6 |
| 3.0 - 4.0 | 4283 | 98.3 |

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kati ya watahiniwa 4,283 (98.3%) waliopata alama 3 hadi 4, kati yao, asilimia 93.1 walipata alama zote 4. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *matumizi na utunzaji wa zana*. Baadhi ya watahiniwa walibainisha faida anazozipata mwanafunzi anapojifunza kwa kutumia zana kama ifuatavyo: *husaidia kutunza kumbukumbu kwa muda mrefu, huamsha ari ya kupenda kujifunza, humrahisishia mwanafunzi kuelewa somo, mwanafunzi kulipenda somo, kukuza na kuibua udadisi, huchangamsha milango ya fahamu*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


10

(i) Kuweza kujifunza kwa urahisi kutokana na zana alizotumia mwalimu kufundishia.

(ii) Humwezesha mwanafunzi kuwa na kumbukumbu ya muda mrefu.

(iii) Humjengea mwanafunzi ari ya kuwa mdadisi wa yale anayojifunza kupitia zana.

(iv) Mwanafunzi kuweza kulipenda somo na hata mwalimu wa somo na kuweza kupata matokeo mazuri kupitia mitihani au majaribio atakayo pimwa.

**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10

Katika Kielelezo Na. 10.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi faida anazoweza kuzipata mwanafunzi anapofundishwa kwa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 2 hadi 2.5 hawakueleza kwa usahihi hoja zilizoorodheshwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yafuatayo: *hutunza kumbukumbu, hukuza uwezo wa kubuni kwa mwanafunzi, hukuza udadisi kwa mwanafunzi* na *wanafunzi hulipenda somo.* Hoja zote ni sahihi lakini mtahiniwa hakutoa maelezo kwa mujibu wa matakwa ya swali, hivyo alipata alama 2 badala ya alama zote 4 katika swali hilo. Majibu hayo yanaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia.

Kwa upande mwingine watahiniwa 2 (0.1%) waliopata alama hafifu hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika kama ifuatavyo: *husaidia kukuza vipaji vya wanafunzi*, *humjengea mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu, huvuta usikivu* na *hufanya wanafunzi kulipenda somo*. Mtahiniwa huyo alitoa majibu sahihi kwa hoja ya pili na ya nne ingawa hakutoa maelezo kulingana na matakwa ya swali. Aidha, hoja ya kwanza na ya tatu hazikuwa sahihi. Mtahiniwa mwingine katika kundi hili, alishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kama inavyoonesha katika Kielelezo Na. 10.2.


10
i) Inarahisisha somo kueleweka kwa urahisi mwalimu anapotumia zana ni sahihi somo kueleweka kwa haraka na ujifunzaji kuwa bure.
ii) Inasaidia mwalimu kujiamini kwa kuwa zana anazo zana ya uhakika, anapoingia darasani ni sahihi kujiamini kwa ujumla.
iii) Inasaidia mwalimu kufikia lengo mahususi ya somo mwalimu anapotumia zana, ni sahihi katika malengo ya somo kwa ujumla na kwa usahihi.
iv) Inasaidia mwalimu kumaliza mada kwa wakati kwa kuwa somo linaeleweka ni sahihi ya mwalimu kumaliza mada kwa haraka au kwa wakati

**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10

Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa aliandika faida za zana kwa upande wa mwalimu badala ya faida za zana kwa upande wa mwanafunzi.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA

Maswali katika sehemu B yalitoka katika mada tano (5) ambazo ni *Zana za kufundishia na kujifunzia, Maandalizi ya maandiko, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia, Maandalizi ya Ufundishaji, Misingi ya kufundishia somo la Haiba na Michezo* na *Upimaji na tathmini ya ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo*. Kila swali lilikuwa na ya alama 15 hivyo
kufanya jumla ya alama 60 katika sehemu hii.

### 2.2.1 Swali la 11: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja tano kueleza changamoto zinazoweza kujitokeza iwapo mwalimu atawapeleka wanafunzi uwanjani bila ya kuwakumbusha sheria na kanuni zinazopaswa kuzingatiwa katika mchezo husika. Jumla ya watahiniwa 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 3,540 (81.3%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 808 (18.6%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 5 (0.1%) walipata alama 0 hadi 5.5. Ufaulu wa swali hili kwa ujumla ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 99.9 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa viwango vya ufaulu katika swali hili ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na.4: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11**

| Alama | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| 0.0 – 5.5 | 5 | 0.1 |
| 6.0 – 10.0 | 808 | 18.6 |
| 10.5 - 15.0 | 3540 | 81.3 |

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kati ya asilimia 81.3 ya watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15, asilimia 24.4 walielewa matakwa ya swali na pia walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa katika kundi hili ni kama: *kuvunjika kwa*

mchezo, kutumia muda pungufu au zaidi, kuumia kwa mchezaji, kuwa na upendeleo, migongano (ugomvi) wachezaji au msimamizi wa mchezo, kupata matokeoambayo siyo halali na kutozingatiwa kwa mchezo wa kiungwana. Kielelezo Na. 11 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa sahihi.

**11**

Sheria ni kanuni zilizowekwa ili kuongoza mchezo.
Kanuni ni utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika
kucheza michezo. Zifuatazo ni changamoto zinazoweza
kujitokeza iwapo mwalimu atawapeleka wanafunzi
uwanjani kucheza bila ya kuwakumbusha sheria na
kanuni za mchezo husika.

Ajali. Hii pia inaweza kutokea iwapo mwalimu
atawapeleka uwanjani wanafunzi kucheza bila kwenda
kuangalia vifaa pamoja usalama wa vifaa na uwanja
ambao wanaenda kutumia katika mchezo husika.

Kuwepo kwa migogoro. Hii inaweza kutokea
iwapo mwalimu atawapeleka uwanjani wanafunzi
kucheza bila kuwakumbusha sheria na kanuni za
mchezo na hivyo kupelekea kukosekana kwa maelewano
baina ya timu au wachezaji katika kucheza mchezo
husika katika uwanja.

Kuvunjwa / kutofuatwa kwa kanuni na sheria.
Endapo mwalimu atawapeleka uwanjani wanafunzi kuche
za bila kuwakumbusha sheria na kanuni za mchezo,
itafanya wanafunzi kuweza kuvunja sheria na kanuni
na mchezo huo ambao wanacheza.

Kukosekana kwa amani na utulivu. Endapo
mwalimu atawapeleka uwanjani wanafunzi kucheza
bila kuwakumbusha sheria na kanuni za mchezo,
itasababisha kukosekana kwa amani na utulivu
uwanjani wakati mchezo unaendelea baina ya
wachezaji au baina timu.

Kukosekana kwa ushirikiano baina ya wachezaji.
Mwalimu endapo atawapeleka uwanjani wanafunzi
kucheza bila kuwakumbusha sheria na kanuni za
mchezo, itapelekea wachezaji kukosa kupeana ushiri



11 Cont. kiano katika mchezo huo na hatimaye kusababisha kushindwa kufanya visuri katika mchezo huo.

Kushindwa kufanya maamuzi yenye busara. Endapo mwalimu atawapeleka wachezaji uwanjani bila kuwa kumbusha kanuni na sheria za mchezo itafanya wanafunzi kukosa /kushindwa kufanya maamuzi yenye busara katika mchezo akiwa uwanjani.

Hivyobasi, Ili kuepukana na changamoto hizi ni vema mwalimu kuwakumbusha wanafunzi kabla ya kuwapeleka uwanjani kanuni na sheria za mchezo husika ili wanafunzi waweze kufuata kanuni na sheria za mchezo, kuwepo na amani na utulivu na kufanyika kwa maamuzi yenye busara na kuweza kujenga ushirikiano katika kucheza mchezo huo.

**Kielelezo Na. 11.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11

Katika Kielelezo Na.11.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi changamoto tano zinazoweza kujitokeza iwapo mwalimu atawapeleka wanafunzi uwanjani bila kuwakumbusha sheria na kanuni zinazopaswa kuzingatiwa katika mchezo husika.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 6 hadi 10 walikuwa na maarifa ya wastani hivyo kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitaja changamoto bila ufafanuzi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *ajali mbalimbali, kutolewa katika mchezo, kushindwa katika mchezo na kupewa kadi, matumizi makubwa ya fedha* na *kutokea kwa ugomvi uwanjani*. Mtahiniwa huyo alieleza kwa usahihi hoja ya kwanza na ya tano, lakini hoja ya pili, ya tatu na ya nne hazikuwa sahihi. Majibu hayo yanaonesha kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa katika swali hili, asilimia 0.1 ya watahiniwa walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kutoelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu yasiyo sahihi kama: *kushindwa kupata ushindi, kupoteza mchezo, kutokukuza stadi za mchezo husika, kupata kadi nyekundu au njano, kushindwa kutoa na kupokea pasi na kukaza kwa misuli*. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

11

~~Ka~~ Sheria, ni kanuni ambazo zimewekwa kwa lengo la kuzitekeleza kwa kufuata taratibu lakini kanuni ni taratibu ambazo zimewekwa ili zitekelezwa kwa mujibu wa sheria zifuatazo ni changamoto zinazoweza kujitokeza kwapo atawapeleka wanafunzi uwanjani bila kuzingatia kanuni na taratibu.

Kukaza kwa misuli, mwalimu akiwapeleka wanafunzi uwanjani bila kuzingatia kanuni na sheria za michezo anoweza akawasababishia wanafunzi wake kukazwa kwa misuli na kushindwa kucheza mpira kwa sababu kabla ya kuanza michezo walimu wanashauriwa wawafanyishe mazoezi ili mwili uwe tayari kwa michezo migumu. hivyo basi, mwalimu asipozingatia kanuni na sheria anaweza akasababisha wanafunzi kukaza kwa misuli.

Kutokwa na damu puani, pia hii ni changamoto ambayo inaweza ikajitokeza kama mwalimu atawapeleka wanafunzi wake kucheza uwanjani bila kuzingatia kanuni na sheria ambazo zimewekwa na nilazima kanuni na sheria hizo zifuatwe kwa lengo la kuondoa changamoto hizo ambazo wanafunzi wako wanaweza kuzipata, hivyo basi kama mwalimu hajazingatia kanuni na sheria za michezo kwa wachezaji wake anaweza akawasababishia kutokwa na damu puani

Kuteguka kwa viungo vya mwili, mfano wa viungo hivyo ni mikono na miguu ni

11 Cont. wajibu wa mwalimu kufuata kanuni na sheria zote za michezo kwa lengo la kutatua au kuepusha changamoto ya kuteguka kwa viungo vya mwili ambavyo husababisha na kutokufuata kanuni na sheria za michezo uwanjani.

Kupasuka kwa misuli, pia mwalimu wa michezo anatakiwa azingatie kanuni za kuwafanyisha wanamichezo mazoezi yote rahisi kabla ya kuanza michezo yenyewe uwanjani kwa lengo la kuepuka changamoto ya kupasuka kwa misuli kwa sababu misuli ikiikaza na kushindwa kurudi katika hali yake ya mwanzo huweza kusababisha misuli hiyo kupasuka hivyo basi mwalimu anatakiwa azingatie kanuni na sheria za michezo.

Kusababisha kifo/vifo kwa wachezaji, mfano mwalimu akawapeleka wanafunzi uwanjani na kuanza kuwakimbiza mbio na efu wanafunzi hao wanaweza wakaishiwa pumzi na kusababisha moyo kushindwa kusukuma damu au kusukuma damu kwa haraka na kupelekea vifo kwa wachezaji.

Hivyo basi, kanuni na sheria za michezo zisipofuatwa humsaidia mwalimu kuepusha hatari kama vile vifo, kukaza kwa misuli, kupasuka kwa misuli na kutokwa na damu puani ninapenda kuwashauri walimu wa michezo kufuata kanuni na sheria za michezo.

**Kielelezo Na. 11.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11

Katika Kielelezo Na. 11.2, mtahiniwa alieleza hoja 5 zinazohusu ajali zinazoweza kujitokeza uwanjani badala ya kueleza changamoto nyingine zinazoweza kujitokeza iwapo mwalimu atawapeleka wanafunzi uwanjani bila kuwakumbusha sheria na kanuni zinazopaswa kuzingatiwa katika mchezo husika.

### 2.2.2 Swali la 12: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza changamoto tano ambazo mwalimu atakutana nazo endapo atafundisha bila kutumia andalio la somo. Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa juu ya matumizi ya andalio la somo. Watahiniwa wote 4,353 (100%) walijibu swali hili kati yao, watahiniwa 2,373 (54.5%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 1,978 (45.5%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 2 walipata alama 0 hadi 5.5. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ni mzuri kwa sababu watahiniwa 4,351 kati ya 4,353 walifaulu swali hili kwa kupata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa viwango vya ufaulu katika swali hili ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na.5.

**Jedwali Na.5: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12**

| Alama | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| 0.0 – 5.5 | 2 | 0.0 |
| 6.0 – 10.0 | 1,978 | 45.5 |
| 10.5 - 15.0 | 2,373 | 54.5 |

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, kati ya watahiniwa 2,373 (54.5%) waliopata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 553 (23.3%) walipata alama 13.5 hadi 14.5, kwa sababu walieleza kwa ufasaha changamoto tano ambazo mwalimu atakabiliana nazo kwa kufundisha bila ya kutumia andalio la somo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika majibu kama vile: *mwalimu kushindwa kufuata hatua za ufundishaji, mwalimu kutojiamini, mwalimu kushindwa kutumia muda vizuri, mwalimu kushindwa kuchagua mbinu za kufundishia, mwalimu kupotosha maudhui na mwalimu kushindwa kuandaa na kutumia zana za kufundishia na kujifunzia*. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

12

Andalio la somo: Ni mpango kazi wa muda mfupi anaoundaa mwalimu na kuuratibu ili aweze kufuata au kuutumia katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la haiba na michezo: Katika kuandaa andalio kuna baadhi ya vitu vya kuzingatia mfano kiongozi cha mwalimu, kitabu cha ziada na kiada pamoja na muhtasari: Zifuatazo ni changamoto au athari za mwalimu kutokuandaa andalio la somo:-

Kutokufikia malengo mahususi: Mwalimu asipo andaa andalio la somo litampelekea mwalimu huyo asifikie malengo mahususi ya somo la haiba namichezo aliyojiwekea katika kipindi kimoja cha dakika 40 ~~and~~ au vipindi viwili.

Mwalimu kutokufundisha kwa mtiririko mzuri: Hii itampelekea mwalimu ambaye hajaandaa andalio la somo fulani kufundisha kwa kutoka nje ya muda pindi anapofundisha: Kwahiyo changamoto atakayo kumbana nayo ni kufundisha bila kufuata mtiririko mzuri wa shughuli aliyotarajiwa kuifundisha.

Kutojiamini wakati anapofundisha: Changamoto nyingi ya kutokuandaa andalio la somo ni kwamba mwalimu ~~atakuwa~~ anafundisha bila kujiamini kwasababu anakuwa hana uhakika na kile anachokifundisha kwahiyo kutoandaa andalio itampelekea mwalimu kufundisha kwa hofu.

Kushindwa kutumia muda wake kwa ufanisi: Athari nyingi ya kutokuandaa andalio la somo katika mchakato wa ufundishaji itampelekea mwalimu kushindwa kujua muda anaotakiwa kutumia katika kipindi hii inamaanisha kwa mwalimu ataweza kutumia muda mchache sana au mwingi sana



12 Cont. pindi anapofundisha bila kuandaa andalio la somo.

Kushindwa kujua zana au vifaa vya kufundishia shughuli fulani anayotakiwa kwenda kufundisha: Kutokana na mwalimu kutokuandaa andalio la somo itasababisha mwalimu huyo kutokujua vifaa au zana zitakazotumika kufundishia somo vizuri na kusababisha kutokueleweka kwa wanafunzi kutokana na kutokuwa na zana za kufundisha.

Kwahiyo: Andalio la somo linatakiwa kila mwalimu aandae kwasababu litamsaidia mwalimu kufundisha kwa kujiamini, kutumia muda wake kwa ufanisi, kushindwa kupanga shughuli za somo katika mtiririko wenye mantiki nakadhalika.

**Kielelezo Na. 12.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12

Katika Kielelezo Na. 12.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi changamoto ambazo mwalimu atakumbana nazo atakapofundisha bila kutumia andalio la somo.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama 6 hadi 10 walikuwa na maarifa ya wastani hivyo, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitaja changamoto bila ufafanuzi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *kufundisha kwa kubabaisha, kufundisha kwa kutojiamini, wanafunzi kutomuelewa mwalimu, mwalimu kuwachosha wanafunzi* na *mwalimu kutofikia lengo la somo*. Katika majibu ya mtahiniwa huyo, hoja ya kwanza na ya pili alizielezea vizuri japo ni hoja zinazofanana. Aidha, katika hoja ya tano mtahiniwa alitoa maelezo kwa ufasaha na hoja ya tatu na ya nne hazikuwa sahihi. Majibu hayo yanaonesha kuwa, mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Andalio la Somo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wawili (02) walipata alama hafifu ambapo mmoja alipata alama 4 na mwingine alama 5. Watahiniwa hao walitoa hoja chache hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa hoja pungufu.

12

Andalio la somo ni mpango kazi anaoandaa mwalimu kabla ya kuingia darasani ambao atapaswa kuutumia kwa kipindi cha dakika arobaini (40) katika mada husika. Zifuatazo ni changamoto zitakazomkumba mwalimu wa Haiba na michezo pale ambapo ataingia darasani kufundisha bila ya kuwa na andalio la somo.

Kutokufikia lengo mahususi; Mwalimu huyu wa somo la Haiba na michezo atakumbana na changamoto yakutokufikia lengo mahususi kwasababu mwalimu atafundisha tu bila ya kuwa na zana wala mbinu ambayo ameiandaa na ambayo itapelekea kumfanya kufikia lengo mahususi.

Mwalimu kufundisha kwa kutumia muda mrefu / kutumia muda vibaya: Hii ni changamoto atakayo kumbana nayo mwalimu huyo kwasababu mwalimu pale ambapo ataandaa andalio la somo kutamsaidia kupanga muda wake vizuri katika ufundishaji wake. Lakini mwalimu huyo pale ambapo atafundisha bila ya kuandaa andalio la somo kutasababisha afundishe bila yakuzingatia muda kwasababu ya kutokuwa na andalio la somo.

**Kielelezo Na. 12.2:** Sampuli ya jibu lenye hoja pungufu katika swali la 12

Katika Kielelezo Na.12.2, mtahiniwa alieleza hoja mbili badala ya hoja tano hivyo, alipata alama 5 kati ya 15 za swali hilo.

### 2.2.3 Swali la 13: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza faida ya wanafunzi kushiriki katika michezo. Lengo la swali hili lilikuwa ni kupima uwezo wa watahiniwa katika kutathmini tija ya michezo katika maisha ya wanafunzi. Watahiniwa wote 4,353 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 4,258 (97.8%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 86 (2%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 9 (0.2%) walipata alama 0 hadi 5.5. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 99.8 ya watahiniwa walifaulu

swali hili kwa kupata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na.6.

**Jedwali Na.6: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13**

| Alama | Idadi ya wanafunzi | Asilimia |
|---|---|---|
| 0.0 – 5.5 | 9 | 0.2 |
| 6.0 – 10.0 | 86 | 2.0 |
| 10.5 - 15.0 | 4258 | 97.8 |

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya Ufundishaji wa Mfano. Miongoni mwao, watahiniwa wawili (2) walipata alama zote 15. Kwa ujumla, watahiniwa katika kundi hili walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya faida za wanafunzi kushiriki michezo na walielewa vema matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja sahihi kama vile: *ni chanzo cha ajira, kukuza vipaji, kujenga afya miongoni mwa wanafunzi, chanzo cha burudani, kujenga ushirikiano, hujenga mawasiliano mazuri kati ya mwanafunzi mmoja na mwingine, huzuia magonjwa kama Presha* na *huondoa msongo wa mawazo.* Tofauti ya alama kati yao ilitokana na utofauti katika kufafanua hoja walizozitoa pamoja na ujuzi katika kuandika utangulizi na hitimisho katika insha zao. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

13 Michezo: Ni muhimu kwa binadamu katika kujenga na kuimarisha akili, mwili na viungo. Zipo aina mbili za michezo ambazo ni michezo ya asili na michezo ya kisasa. Ushiriki wa michezo kwa wanafunzi una tija sana katika maisha yao.

Yafuatayo ni umuhimu wa wanafunzi kushiriki katika michezo

Michezo huibua vipaji: Wanafunzi wanashiriki katika michezo mbalimbali inasaidia kuibua vipaji na kuwa wachezaji wazuri au wakubwa wa baadae ivyo ni muhimu wanafunzi kushiriki katika michezo kwa kuwa ina tija sana katika maisha yao kwa kuwa huibua vipaji.

Michezo hujenga afya ya akili: Pia michezo inasaidia kujenga afya ya akili hivyo ni muhimu wanafunzi kushiriki katika michezo mbalimbali mfano mpira wa miguu, mpira wa mikono, mbio, mpira wa kikapu michezo hii inawasaidia kujenga afya ya akili. Hivyo michezo ina tija sana katika maisha yao.

Michezo huimarisha viungo vya mwili: Wanafunzi wanaposhiriki katika michezo inawasaidia viungo vyao vya mwili kuimarika mfano misuli ya mikono, miguu inawasaidia wanaimarika na kuwa watakamavu kutokana na kushiriki katika michezo mbalimbali mfano kukimbia, kuruka kamba, kutembea, kunyanyua vitu vizito vinasaidia kuimarisha viungo vya mwili. Hivyo michezo ina tija sana katika maisha yao.

Michezo husaidia kujikinga na magonjwa: Pia michezo wanafunzi wanaposhiriki katika michezo mbalimbali husaidia kuepukana na magonjwa mbalimbali mfano mafua, ongezeko la mafuta mwilini kuwa na manyama uzembe hupungua hivyo michezo husaidia kujikinga na magonjwa nyemelezi. Hivyo michezo ina tija sana katika maisha yao.


13 Cont. Micheeo hubunidisha : Pia michezo huwabunidi
cha wanafunzi iwapo wataunda timu na kushinda kisha ku
pata ushindi hili ni moja wapo ya umuhimu wa micheoo wana
funzi hubunidika Mfano Watakaposhinda michezo na shule jirani
inawajengea wanapata burudani. Hivyo michezo ina tija sana kati
ka maisha yao.
Kwa kuhitimisha : Tumeona kuwa michezo ina ti
ja sana kwa maisha ya wanafunzi kwa kuwa huibua vipaji M
ichezo hubunidisha, Michezo hujenga afya ya akili, Michezo huima
risha nungo ya mwili, Pamoja na michezo husaidia kujikinga
na magonjwa mfano mafua.

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 13

Katika Kielelezo Na. 13.1, mtahiniwa aliandika kwa usahihi faida za michezo katika maisha ya wanafunzi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 6 hadi 10 walikuwa na maarifa ya wastani hivyo, walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine walitaja faida bila ufafanuzi wa kina. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *michezo ni chanzo cha kipato, michezo humfanya mwanafunzi kuwa mkakamavu, michezo huwezesha kujenga afya, michezo huwajengea wanafunzi moyo kujiamini,* na *husaidia wanafunzi kuhusianisha maarifa.* Mtahiniwa huyo alifafanua hoja zote ingawa hoja ya kwanza, ya tatu na ya nne ndizo zilikuwa sahihi. Hoja ya pili ni marudio ya hoja ya tatu na hoja ya tano haikuwa sahihi.

Pamoja na watahiniwa kufanya vizuri katika swali hili, asilimia 0.2 ya watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana iliyoulizwa na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi hivyo walipata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama: *husaidia wanafunzi kujiwekea malengo, husaidia wanafunzi katika kuandaa timu, huelimisha jamii na humfanya mwanafunzi kurekebisha tabia*. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mmoja wa watahiniwa.

13 Michezo ni somo linalohusika na viungo vya mwili pamoja na utumiaji wa matendo na akili. Kuna michezo mbalimbali ambayo wanafunzi huwa wanashiriki kama vile mpira wa miguu, mpira wa pete, kuruka kamba, mdako, na mpira wa kikapu hiyo ni baadhi ya michezo ambayo wanafunzi hushiriki. Zifuatazo ni sababu zinazowafanya wanafunzi kuwa na tija katika ushiriki wa michezo mbalimbali

Kutopatiwa elimu kuhusu michezo, wanafunzi wengi huwa wanashiriki katika michezo lakini hawana elimu kuhusu mich ezo ambayo wanaicheza na ndio maana wanafunzi wengi huwa na tija katika michezo kwa sababu wanakua hawajui umuhimu wa michezo kwa mfano michezo ni ajira, hukuza ushirikiano, huibua vipaji mbali mbali. na michezo huimarisha viungo vya mwili. Endapo wanafunzi watapatiwa elimu kuhusu michezo kutakuwa hakuna changamoto yoyote ambayo itawafanya wao wawe na tija kushiriki michezo.

Kutokuwa na vifaa vya michezo, mfano mipira, jezi na uwanja na ndio maana wanafunzi wengi hawapendi kushiriki michezo kutokana na kukosekana kwa wazamini kati ka kuwapatia vifaa vya michezo. Ni muhimu kwa wanafunzi kuwa na vifaa vya michezo ambavyo vitawahamasisha wao kuwa na tija ya kushiriki michezo mbalimbali kama vile mpira wa miguu, mpira wa pete, mdako na kuruka kamba.

13 Cont.

Kutokuwa na wazamini katika michezo,
wazamini wa michezo mbalimbali ni muhimu
kwa sababu wanakuwa wanatoa hamasa ya
wanafunzi kushiriki michezo mbalimbali. Wazamini
wa michezo ni muhimu kwa sababu huwa
wanahusika na utoaji wa tuzo katika michezo
na kuwafanya wanafunzi wawe na tija ya kutaka
kushiriki michezo mbalimbali kama vile
mpira wa pete, mpira wa miguu, mpira wa
kikapu na kuruka kamba endapo kutawa na
wazamini mbalimbali kutawasaidia wanafunzi
kuwa na hamu ya kushiriki michezo mbalimbali.
Kutokuwa na ushirikiano wakati
wa michezo, baadhi ya wanafunzi waliowengi
wanashindwa kuwa na hamasa ya kushiriki
michezo kwa sababu hawana ushirikiano mio
ngoni mwao na ndio maana hawaoni umuhimu
wowote wa kushiriki michezo mbalimbali
kama vile mdako, kuruka kamba, mpira wa
pete, mpira wa kikapu na mpira wa miguu.
Hivyo ni muhimu kwa wanafunzi kuwa na
ushirikiano katika michezo ili waweze kuwa
na hamasa ya kushiriki michezo mbalimbali
Kutopatiwa motisha wakati
wa michezo mfano kupatiwa tuzo na zawadi
kwa walo ambao wamefanya vizuri ili
waweze kuendelea kufanya vizuri Na ndio
maana wanafunzi wengi hawana tija ya
kushiriki michezo mbalimbali kwa sababu
hawapatiwi zawadi na tuzo kwa wanaofanya
vizuri. Zawadi na tuzo zinamfanya mwanafunzi
ambaye hashiriki michezo naye awe na

**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 13

Katika Kielelezo Na. 13.2, mtahiniwa alieleza sababu za wanafunzi kutopenda kushiriki katika michezo mbalimbali badala ya kueleza faida wanazozipata wanafunzi pindi wanaposhiriki michezo mbalimbali.

### 2.2.4 Swali la 14: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja tano kueleza umahiri ambao mwalimu wa somo la Haiba na Michezo anapaswa kuwa nao kumwezesha kuandaa somo lake kwa ufanisi. Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutumia maarifa aliyonayo katika kuandaa somo lake kwa ufanisi. Watahiniwa wote 4,353 (100%) walijibu swali hili ambapo watahiniwa 2,407 (55.4%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 1,821 (41.8%) walipata alama 6 hadi 10 na watahiniwa 123 (2.8%) walipata alama 0 hadi 5.5. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa sababu asilimia 97.2 ya watahiniwa walifaulu kwa kupata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa viwango vya ufaulu katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15 walieleza umahiri ambao mwalimu wa somo la Haiba na Michezo anapaswa kuwa nao. Tofauti ya alama kati yao ilitokana na usahihi wa maelezo ya kila mmoja katika kutetea hoja zake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama ifuatavyo: *awe na uwezo wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia, awe na uwezo wa kuhusianisha somo na mazingira, awe na umahiri wa kutosha katika somo lake, awafahamu*

*wanafunzi wake* na *awe na mbinu bora za kufundishia*. Kielelezo Na.14.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**14**

Somo ni maudhui anayo yaandaa mwalimu kabla ya kwenda kufundisha ili kuweza kumpatia maarifa ya ziada wakati wa kufundisha wanafunzi darasani. Ufuatao ni umahiri ambao mwalimu anapaswa kuwa nao ili kuweza kuandaa somo lake kwa ufanisi.

Mwalimu anapaswa kuielewa mada vizuri; Mwalimu anapoandaa somo kwa ajili ya kwenda kufundisha anapaswa kuielewa mada yake kwa ufanisi ili aweze kuwafundisha wanafunzi wake kwa ubora zaidi.

Kulielewa darasa au wanafunzi vizuri; Mwalimu anapaswa kulielewa darasa lake vizuri au anapaswa kuwaelewa wanafunzi wake ambao ataenda kuwafundisha vizuri na kwa ufanisi hii ita msaidia kubaini changamoto atakazo kutana nazo wakati wa kuwafundisha.

Zana za kufundishia na kujifunzia; Mwalimu anatakiwa kuwa na ujuzi wa kuandaa zana ambazo zitamsaidia ~~wa~~ kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo lake kwa usahihi. na kusaidia kubunza kumbukumbu kwa wanafunzi.

Mbinu za kufundishia; Mwalimu anapoandaa somo anapaswa kujua au kuwa na mbinu mbalimbali ambazo atazitumia kuwafundisha wanafunzi wake ili waweze kumuelewa


14 Cont. kwa urahisi.
Zana za upimaji; Mwalimu anapa-
swa kuwa na umahiri wa kuandaa za-
na za upimaji ambazo zitamsaidia
katika kubaini ni kwa kiasi gani wanafu-
nzi wake wameweza kumuelewa kwa ufa-
saha wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.
Hivyobasi; Mwalimu wa Somo la Haiba
na michezo anapaswa kuwa mahiri wakati
wa kuandaa somo lake kwa ufanisi ili kuwe-
ze kumsaidia kutimiza ufundishaji na uji-
funzaji ulio kusudiwa.

**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 14

Katika Kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa alieleza kwa usahihi umahiri ambao mwalimu wa Somo la Haiba na Michezo anapaswa kuwa nao ili kumwezesha kuandaa somo lake kwa ufanisi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama 6 hadi 10 walikuwa na maarifa ya wastani hivyo, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitaja hoja bila ufafanuzi wa kina. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika; *umahiri katika kuandaa somo, umahiri wa kuwasiliana, umahiri wa kushirikiana, ubunifu wa kuandaa zana* na *umahiri wa uthubutu.* Majibu ya mtahiniwa yalifafanuliwa vizuri ingawa hoja sahihi ilikuwa ni hoja ya kwanza na ya nne wakati hoja ya pili, ya tatu na ya tano hazikuwa sahihi.

Pamoja na watahiniwa kufanya vizuri katika swali hili, asilimia 2.8 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 5.5. Baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha na wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Uthibitisho wa majibu yaliyotolewa na mtahiniwa mmoja ni: *mwalimu awe na umahiri wa kubaini maneno mbalimbali katika picha, awe na stadi za maisha, stadi ya kuchonga, stadi ya kuchora* na *stadi ya uthubutu,* hoja hizo hazikuwa sahihi. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama; *stadi ya kujiamini, stadi ya maandishi, umahiri katika kuunda, stadi za mawasiliano, stadi ya udadisi na stadi ya ubunifu*. Hoja hizo hazikuwa sahihi hivyo kusababisha watahiniwa kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

14

Umahiri; ni ujuzi anaokuwa nao mtu katika kufanya jambo fulani. Kwa hoja tano, nadharia umahiri anaopaswa kuwa nao mwalimu wa somo la Haiba na Michezo ili kumwezesha kuandaa ~~a~~ somo lake kwa ufanisi

Lielewekao (specific) Katika uandaaji wa somo, ili liwe na ufanisi hupaswa kuwa katika mpangilio unaotakiwa katika maudhui ili mwanafunzi awe na kuelewa vizuri.

Lipimike; Ili mwalimu aweze kuandaa somo lake kwa ufanisi, somo linatakiwa liwe na vipimo yaani kuwe na kiwango katika ufundishaji na hii kumsaidia mwanafunzi kuelewa zaidi na kuepuka pia kumchanganya mwanafunzi

Liafikiwe; Katika uandaaji wa somo, mwalimu wa somo hupaswa kufikia mwafaka, ili kumwezesha kuweza kuendelea na kipengele kingine katika ufundishaji wake.

Uhalisia; Katika uandaaji wa somo, mwalimu hupaswa kuhusianisha somo na mazingira halisi ili mwanafunzi aweze kuona wepesi katika somo na pia mwalimu huwe za kutumia zana halisi kama kielelezo katika ufundishaji wake.

Muda; Mwalimu hupaswa


14 Cont. kuzingatia muda katika ufundishaji wake ili kuepuka kufundisha mambo mengi kwa wakati mmoja na pia kuepusha kumchanganya mwanafunzi. Hivyo basi Mwalimu asipozingatia tarahibu katika kuandaa somo lake humpelekea kutofikia lengo alilokusudia (mahususi), wanafunzi kutolipenda somo.

**14.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14

Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa alieleza sifa za malengo mahususi katika andalio la somo badala ya umahiri ambao mwalimu wa somo la Haiba na Michezo anapaswa kuwa nao ili kumwezesha kuandaa somo lake kwa ufanisi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU KATIKA KILA MADA

Kati ya mada tano zilizotahiniwa katika somo la Haiba na Michezo, mada nne zilikuwa na ufaulu mzuri. Mada hizo ni: *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* (98.8%), *Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia* (89%), *Maandalizi ya Ufundishaji* (77.4%) na *Misingi ya Kufundishia Somo la Haiba na Michezo* (76.2%). Mada ya *Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Haiba na Michezo* ilikuwa na ufaulu wa wastani (56.1%). Ufaulu mzuri katika mada hizi ni matokeo ya watahiniwa kuwa na uelewa mzuri katika mada husika. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa katika mada zilizotahiniwa umewasilishwa katika Kiambatisho cha Pekee.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika somo hili ni mzuri kwa kuwa asilimia 100 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Sababu zilizo chagiza ufaulu mzuri ni pamoja na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali walizotahiniwa, umahiri wa kutosha katika kuandika hoja zenye mtiririko mzuri, kusoma na kuelewa matakwa ya swali. Hata hivyo, ili kuimarisha zaidi na kuendeleza ufaulu mzuri katika somo la Haiba na Michezo kwa mitihani ijayo, juhudi zaidi katika matumizi ya njia shirikishi za ufundishaji zinahitajika, ufundishaji uhusishe nadharia na vitendo (walimu tarajali wapewe fursa zaidi za kucheza michezo mbalimbali), utoaji wa mazoezi ya kutosha ili kuimarisha ujifunzaji wa walimu tarajali hususani katika mada ya *Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo* ambayo ilikuwa na ufaulu wa wastani.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuongeza ufaulu zaidi katika mada zilizofanya vizuri na kupandisha ufaulu katika mada ya *Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo* iliyokuwa na ufaulu wa wastani, yafuatayo yanapendekezwa;

(i) Walimu tarajali wapewe kazi nyingi zaidi zitakazochochea ujifunzaji wakati wa ufundishaji. Aidha, majaribio ya mara kwa mara pamoja na mitihani itolewe sambamba na kutoa mrejesho wa haraka ili kuwajengea walimu tarajali namna bora ya kujibu maswali.

(ii) Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji uzingatie njia shirikishi kama vile changanya kete, ziara za kielimu, majadiliano kwenye vikundi na igizo dhima. Lengo ni kuwajengea zaidi walimu tarajali na kuwa mahiri katika kufikiri na kutoa maelezo kwa ufasaha.

(iii) Walimu tarajali wanashauriwa kusoma zaidi vitabu mbalimbali, majarida na machapisho mengine kwa lengo la kujiongezea maarifa na kuwa mahiri katika somo la Haiba na Michezo.

(iv) Mchakato wa ufundishaji uhusishe nadharia na vitendo. Mbali na kujifunza nadharia mbalimbali wanachuo pia washirikishwe katika kujifunza kwa vitendo ndani ya darasa na nje ya darasa. Vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia vitumiwe na wanachuo ili kuwawezesha kujifunza kwa vitendo na kuwa mahiri zaidi katika mada wanazojifunza.

(v) Somo la Haiba na Michezo lifundishwe katika Shule zote za Msingi ili kuwawezesha walimu tarajali kufanya mazoezi ya kufundisha somo hili wakiwa katika mafunzo kwa vitendo ya muda mrefu. Hii itawafanya wawe mahiri zaidi katika kutumia maarifa waliyopata darasani kwenye mazingira halisi hali itakayopelekea kuwa na ufaulu mzuri

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ZA SOMO LA HAIBA NA MICHEZO

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Ufaulu Katika kila Swali (asilimia) | Wastani wa Ufaulu katika kila Mada (asilimia) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 8 | 97.7 | 98.8 | Vizuri |
| | | 10 | 99.9 | | |
| 2. | Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 3 | 99.9 | 89 | Vizuri |
| | | 7 | 69.9 | | |
| | | 14 | 97.2 | | |
| 3. | Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo | 4 | 44.3 | 77.4 | Vizuri |
| | | 9 | 43.3 | | |
| | | 11 | 99.9 | | |
| | | 12 | 99.9 | | |
| | | 13 | 99.8 | | |
| 4. | Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo | 2 | 82.3 | 76.2 | Vizuri |
| | | 6 | 70.1 | | |
| 5. | Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo | 1 | 97.3 | 56.1 | Wastani |
| | | 5 | 14.8 | | |